Jiwe la kiroho la kujenga no: 25

# LAKINI IJAPO ILE ILIYO KAMILI

*1-Wakorinto 13:10, lakini ijapo ile ilio kamili ilio kwa sehemu itabatilika.*

Kwa hiyo haya mambo madogo ya kuruka juu na chini kama mtoto kujaribu kuzungumza kwa lugha na mambo mengineyo kama hayo ijapo ile ilio kamili ………na leo kwa msaada wa Mungu tunayo tafsiri kamilifu ya neno la Mungu likithibitishwa na Mungu mwenyewe kwa hiyo sasa ile iliyo kuwa sehemu itabatilika, nilipo kuwa mtoto mchanga nalifikiri mtoto mchanga , na ali sema kama mtoto mchanga , nalifahamu kama mtoto mchanga tokea hapo nilipokuwa mtu mzima nimeyabatilisha mambo ya kitoto (1-wakorintto13;11) amina. Tafadhali hebu elezea 1-wakorintto 13;8-12 sasa neno kamilifu limerejeshwa kanisani hii mistari imetimia? sasa nafikiri nimepatia hivyo si ndio hivyo na ijapo ile ilio kamili ile ilio kuwa sehemu itabatilika, Paulo alisema ijapo na sema kwa lugha ya mwanaadamu na za Malaika na kufanya haya mambo mengineyo hapo ………. Lakini ijapo ile iliyokamili……sasa kuna kitu chochote kilicho kamilifu isipokuwa Mungu? hapana bwana, Mungu ndie mkamilifu, hapo mwanzo kulikuwako neno naye neno alikuwako kwa Mungu, na neno alikua ni Mungu (Yohana 1;1) neno bado ni Mungu unaona? vema ijapo ile ilio kamili, ile iliyo kwa sehemu itabatilika [1]

Unalipata hilo Amina, kwa maana Mungu alisema nitawarudishia hilo yeye ataenda kulirejesha kwa namna gani? wajumbe wanne wa mauti waliliua hilo halafu wakaja wajumbe wenye uhai wanne kulirejesha hilo, wakwanza alikuwa ni nani? Martin luther kuhesabiwa haki kwa amani, wa pili alikuwa ni nani? John wesley utakaso, watatu alikuwa ni nani? Pentekoste pamoja na kurejeshwa vipawa na Roho mtakatifu, ubatizo wa Roho mtakatifu, wa nne alikuwa ni nani? Ilikuwa ni neno, nini, neno? [2]

Angalia hapa ule uhai aliokua kwenye suke kwenye bua, kwenye kapi katika suke wote huo ulijikusanya kwenda kwenye mbegu, na uhai uliokua kwenye bua uliondoka, moja lilienda kutengeneza lingine kule kuhesabiwa haki kuliweka njia kwaajili ya utakaso, utakaso uliweka njia kwa ajili ya Roho mtakatifu mwenyewe. Kuja katika ukamilifu unaturudisha tena kwenye neno ilikujidhihirisha lenyewe. [3]

Kunapo kuwepo na lugha, zitakoma, kunapo kuwepo na maarifa yatakwisha, kunapo kuwepo imani itashindwa na mambo mengine, hapo lakini ile iliokamili ikija ambayo ni upendo (1-Yohana4:7-8;16) kamwe haitapita hiyo ni sawa upendo wa Kristo. [4]

Lakini ndugu kama unanena kwa lugha na halafu ukaendelea kuishi maisha ambayo ulikuwa unaishi huko nyuma hapo sasa kuna kasoro na ushuhuda wako jambo moja pekee unajifunza juu hapo ni kuzungumza kwa ligha usijaribu kufanya hilo utaanguka pale kwenye maporomoko huo mtumbwi hauta weza kustahamili hayo, zikiwako lugha utakoma, ikiwapo unabii utashindwa lakini japo ile ilio kamili……..oh ule upendo wa Mungu ulivyo msafi na utajiri mwingi hauelezeki na una nguvu ……..hapo sasa hizi karama nyengine zitaenda kazi kwa usahihi pakiwa na hilo unaona? hivyo ni vipawa vya Roho mtakatifu ambavyo umepewa wewe

kuzungumza kwa lugha kutoa unabii, na nini tena na kutafsiri hivyo vyote ni kwaajili ya kujenga kanisa kwa ajili ya kuufanya ule mwili (1-Wakorintho 14:12) lakini cha kwanza umpokee Roho mtakatifu na kwamba uone maisha yako yamebadilishwa (1-Wakorintho 12:13). [5]

Ningetamani kila mshirika wa kanisa langu anene kwa lugha ningetamani hao wafanye na naamini kama utamuomba Mungu , Mingu atakupa hilo lakini hebu niwaambieni kitu nina jua watu wengi wanao nena kwa lugha na hawana Roho mtakatifu na hakuna mhuduma ambaye ni mkweli kwa nafsi yake kusanyiko lake ambae atawaambia watu wake jambo hili hili shetani anaweza akaigiza hilo, Paulo alisema ninapo nena kwa lugha za wanadamu na za malaika niutoe mwili wangu niungue moto kama sadaka hata kama ningejua siri zote za neno la Mungu, hata ningetoa mali zangu zote kuwapa maskini na mambo haya yote kama sina upendo bado mimi si kitu, ningekuwa na imani kuweza kuhamisha milima na kadhalika bado si kitu, halafu akasema ile iliyokuwa sehemu itatoweka ikija iliyo kamili au iliyo kamili ikifahamika. [6]

Sasa Paulo alisema hilo katika (1-Wakorintho 13), jambo linalofatia akasema sasa hata ninge nena kwa lugha za wanadamu na zamalaika (hapo inamaana aina zote za lugha) na kama sina upendo mimi si kitu hata ningekuwa na hekima…...sasa alikua anazungumza juu ya vipawa vilivyopo hapa kwenye mwili kuwa na vipawa bila kua na mtoa vipawa unaona? hata ningekuwa na hekima nakuelewa maarifa yote ya Mungu maandiko yote kuweza kuyaunganisha kama thelojia mkuu, na kama sina upendo ambao ni Roho mtakatifu sikitu mimi. Sasa tunajua kwamba Roho mtakatifu ni Mungu (Yohana 4:24) inabidi tukubali hilo unaona? huyo ni Mungu vema sasa Mungu ni upendo (1-Yohana 4:16) unaona? kwahiyo unaweza ukawa na vipawa na vipawa vyote vya Mungu bila yakuwa na Mungu, Mungu ni upendo, shetani anaweza akaigiza vipawa vyote hivo unaona? anaweza akainiza karibu kila kitu kwasababu anapotosha dhambi na kitu sahihi kina potoshwa. [7]

Sasa hapa haijalishi uko sahihi kiasi gani, hapa kuna jambo moja ambalo tunashindwa na tunalikosa ndugu zangu, haijalishi niko sahihi kiasi gani, haijalishi ninajua maandiko kiasi gani na ni kiasi gani ninajua Biblia ya Mungu kama sina Roho wa Mungu wa upendo katika moyo wangu (Warumi 5:5) kwaajili ya wanadamu wote, hapo sasa kwa kuanzia siko sahihi sasa kama najua siri zote za Mungu na kuzichanganua ziweze kulingana vizuri na kama sina upendo itasaidia nini? [8]

Mimi si chochote mpaka upendo umekuja ndani; upendo wa Mungu, upendo ni neema ya Mungu inayofanya yote. [9]

Kwahiyo mpate Kristo moyoni mwako hiyo ni halisi Kristo na Roho mtakatifu ni mtu huyo huyo. Roho mtakatifu Kristo maana yake ni mpakwa mafuta na Roho mtakatifu ni ule upako na wewe ndiye unapakwa mafuta unaona? Na ni Kristo ndani yako anaekupaka mafuta, unaona ninachomaanisha hapo, sasa una kitu sahihi, hapo sasa anaweza akakutumia kwa kitu chochote anachotaka kukutumia, kwasababu upo katika mwili na unaweza kutumika kwa kipawa chochote (1-Wakorintho 12) lakini unaona kua na moja wapo ya hivyo vipawa nje ya mwili wa Yesu kristo, haitakufanya chochote kizuri usitegemee hayo mambo, Roho mtakatifu ni kiumbe, Mungu ndani yako ile nafsi ambayo imekuosha wewe utu wako wote umebadilishwa, umekuwa kiumbe

kipya(2-Wakorintho 5:17) jambo lolote dogo ambalo si sahihi atakuambia liache usilifanye hilo, baba simaanishi kufanya hilo naomba unisamehe mimi unaona? na huyo ni Roho mtakatifu. [10]

Na ningetoa mali zangu zote kuwalisha maskini ………..ningetoa mwili wangu kuungua moto kama sina hainisaidi kitu, umeona kazi zako zote nzuri, unaona matendo yako yote mazuri vitu vyote vya kiroho ulivyo navyo, misisimko yote uliyo nayo, furaha zote ulizo nazo, haihusiki na chochote cha hayo uliyo yatenda wewe kwa kuanzia, fikiria hilo kwa muda kidogo, angalia vipawa hivi vyote, mambo yote haya mazuri nina walisha maskini nina moyo mzuri mimi ninafanya hili, ninafanya lile, ninaenda kanisani, nina nena kwa lugha, natoa unabii, naponya wagonjwa, nina hubiri injili, (Mathayo 7:21-23) ninafanya mambo haya yote Paulo alisema bado mimi si kitu, mambo haya yote yanaweza yakawa uigizaji wa kimwili, ukarimu, upendo,upendo ni nini? upendo ni Mungu, Mungu anakujaje kwako? kwa kuzaliwa unaona. (Yohana 3:3-8). [11]

Roho mtakatifu anakuja chini kwa uzuri kutuogesha sisi katika ukuu wa uzuri wake, uliokua umevuviwa kuzungumza hayo maneno kwambwa siku moja ya utukufu karama zote zilizopo kanisani zitawekwa pembeni kama ilivyokua zamani na roho mtakatifu mwenyewe atalichukua kanisa katika utawala wake wa upendo wakiungu kiasi kwamba wagonjwa watapona, vipofu wataona, viwete watatembea, bila kuwekewa mikono juu yao utakua ni umoja mkuu. [12]

Upendo halisi husahihisha na unakuleta wewe kwenye neno la Mungu. [13]

Jambo kuu la umuhimu mpende Mungu na ujinyenyekeshe mwenyewe pamoja na hilo. [14]

Mungu ndiye anaeweza kukupa hilo halafu upendo unaleta ushirika. Siku ile ambayo dhambi imetenganisha upendo wa kiungu. Mungu alimuambia adamu na hawa msile aina fulani ya matunda nao wakala dhambi ikaleta utengano na dhambi ilipo leta utengano ikaleta chuki, ikaleta wivu, ikaleta ugomvi ikaleta fitina, hiyo ni kweli? Kulitokea nini? Walijitenga kutoka kwenye upendo wa kiungu na wapo hapo huwezi ukashindwa kuona makosa ya ndugu yako tena inabidi umsimange kwaajili ya haya (1-Yohana 2;10), hiyo nikweli huwezi ukashindwa kuyaona makosa ya dada yako tena kwasababu umeondoka kwenye ule upendo wa kiungu ile sehemu ya kiungu lakini kama unampenda kweli bwana yesu kama dada au ndugu akikufanyia jambo fulani oh vema iyo ni sawa tu hakumaanisha kufanya hivyo hiyo ndiyo aina ya upendo kristo aliokua nao baba uwasamehee hao hawajui wanachofanya (Luka 23;34). [15]

Na ndugu tumejichorea viduara vidogo vya sheria na mambo tofauti na bado hatujafika kwenye kiini halisi ni yesu kristo upendo wa Mungu ambao Mungu anapenda tuone nikitu cha kusikitisha namna gani, upendo ndio silaha yenye nguvu sana ambayo dunia imewahi kuifahamu dunia inakufa kwakukosa upendo, kanisa linakufa kwa upendo wa Mungu, maji ya neema yatiririkayo mmoja kwa mwengine kuaminiana kunaporudishwau haki inaporudishwa kati yetu, Upendo wa Mungu ulio mwagwa kwetu katika mioyo yetu kwa madhebu ……… Kitu flani hapo kimesikika vibaya au sivyo? Upendo wa Mungu umemiminwa mioyoni mwetu kwa Roho mtakatifu (Matendo 5;32) upendo Mungu kwetu…[16]

Hiyo ndiyo sababu ambayo nataka kuweka maisha yangu yote kwaaji ya bwana Yesu kila kitu ninachoweza kufanya kwaajili yake na ninaweza kumtumikia yeye ninapoweza

kuwatumikia watu wake mnaweza kumpenda yeye kadri mnvyopendana mmoja kwa mwingine, ninaweza kumpenda yeye kama tu ninavyoweza kuwapenda ninyi, na pamoja tuna mpenda Mungu na hapo tuna kuwa watoto wake katika hili la kwamba nina kutumikieni ninyi na ninyi mna nitumikia mimi na kwanamna hiyo tunamtumikia Mungu.Yesu alisema kwa kadri mlivyomtendea mmoja wa wadogo hawa mmenitendea mimi (Mathayo 25;40) kwahiyo kama tunataka baraka hebu tuwe baraka kwa mtu fulani na baraka zita turudia,kama kuutupa mkate wako kwenye maji utakurudia na hiyo ni kweli katika maisha haya utaliona hilo mara nyingi unavuna kile unachopanda (Wagalatia:7-10) kwahiyo hebu tufanye mema tuzungumze mema tuwe wakarimu na watu wanapozungumza kuhusu sisi,sisi tuzungumze mambo mazuri,na mambo yaukarimu na mambo mazuri yatakuja kwenye njia yetu kama tuta yatoa. [17]

Sasa mnapenda mimi niwaambie kile ninacho fikiria kitu kikuu sana chenye nguvu ambacho kipo hapa duniani,nguvu iliyokuu ambayo ipo hapa duniani ni upendo,hivyo ndivyo hasa.hakuna chochote ambacho kitavunja upendo haijalishi ni nini,chochote kile ulicho au chochote ulichoimba,unaweza ukawa umecheza katika roho unaweza ukawa amezungumza kwa lugha,unaweza ukawa umepeana mikono na wazee,unaweza ukawa umebatizwa mara tatu,unaweza ukawa kwa upande wa nyuma na kwa upande wa mbele vyovyote upendavyo lakini mpaka upendo uweke nanga moyoni mwako utakua bado uko nje ya Mungu hiyo ni sawa inabidi uwe na upendo, Biblia inasema Mungu ni pendo, upendo ni nguvu kuu. [18]

Hao watu waliokufa katika Kristo, wanatutegemea na kutungoja sisi, kwaiyo ili kanisa linabidi lije kwenye ukamilifu ili kuleta ufufuo, (Waebrania11:39-40,12:1) na nafsi zao ziko madhabahuni zikingojea hili kanisa lifikie kwenye ukamilifu wake na hapa juu kwenye kifuniko cha piramidi kinapokuja ile piramidi yenyewe mwili wa Yesu Kristo inabidi uchongwe (2- Petro 1;3-11) siyo kitu kama kanuni au fundisho au kitu fulani ambacho tumepitia inabidi iwe kamilifu kama Kristo mpaka anapokuja yeye na hiyo huduma vitaingiliana pamoja hapa sasa utakuja unyakuo kule kwenda nyumbani. [19]

**Nukuu za Kiingereza**

[1] "Maswali na majibu (64-0823E)," COD Uk . 1005,1030,1017 ,aya57,164,96-97

[2] "Kule kurejeshwa kwa mti wa bibiarusi" (62-0422),aya505

[3] "kile kiapo" (64-0705),aya 136

[4] "Dhambi isiyo sameheka" (54-1024),aya 118

[5] "Mungu asiye badilika akitenda katika njia isiyotegemewa" (62-0120),aya E-92

[6] "Ule mjadala juu ya kunena kwa lugha" (60-0807),aya E-7

[7] "Kuelezewa kwa unguu" (61-0425B),aya 36

[8] "Ujumbe wa neema" (61-0827),aya 145

[9] "Maswali na majibu" (64-0830M),COD uk 1097

[10] "Wakorintokitabu cha masahihisho" (57-0414),aya E-2

[11] "Ndipo yesu akaja"  (57-0407E),aya E-5

[12] "Kumiliki malango ya adui baada ya kujaribiwa" (64-0322),aya 148

[13] "Jinyenyekeshe mwenyewe"  (63-0714E),93

[14] "Njia ya kupata ushiriki"  (55-1009),aya E-33

[15] "Msikieni yeye" (57-0322),aya E-51

[16] "Sheria" (55-0115),aya E-17

[17] "Je sasa unaamini ?" (55-0610).aya 26

[18] "Kimo cha mtu mkamilifu" (62-1014M),aya 367,371

---

Jiwe la kiroho la kujengea kutoka kwenye neno lililofunuliwa la saa, Imekusanywa na Gerd Rodewald Friedsfr.69,D-75328 Schomberg, Germany
www.biblebelievers, Fax (+49)72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098.*